



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA KIBONDO



TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA KIPINDI CHA MWEZI JANUARI, 2021

A).UMBILE LA BAJETI KWA MWAKA

Katika kipindi cha mwaka wa fedha **2020/2021** Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo imekisia kukusanya na kutumia Tshs **34,161,980,829.46** kutoka katika vyanzo mbalimbali vilivyo kasimiwa katika kipindi cha mwaka pamoja na bajeti timilizi ya mwaka **(2019/2020)** ya Tshs.**1,158,804,754.50** hivyo kufanya jumla kuu ya mapato na matumizi tarajiwa kwa mwaka kufikia Tshs.**35,320,785,583.46** Mchanganuo wa bajeti ya mapato na matumizi kwa mwaka ni kama jedwali **A** linavyoonesha:-

JEDWALI A: MUHTASARI WA BAJETI YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2020/2021

NA.	CHANZO CHA MAPATO NA MATUMIZI	BAJETI (TZS.)
I.	Vyanzo vya ndani (own Source)	1,500,000,000.00
II.	Vyanzo lindwa (CHF,NHIF,DRF,USER FEE,ADA & MICHANGO)	1,208,979,600.00
III.	Ruzuku ya Mishahara (P.E)	15,964,966,232.00
V.	Ruzuku ya Matumizi mengineyo (OC)	3,126,223,360.00
III.	Ruzuku ya Miradi ya Maendeleo (Development Grant)	12,361,811,637.46
	JUMLA YA MAKISIO	34,161,980,829.46
	BAJETI TIMILIZI YA MWAKA (2019/2020)	1,158,804,784.31
	JUMLA YA BAJETI (BAJETI TIMILIZI + MAKISIO)	35,320,785,583.46

B) TAARIFA YA MAPATO-MWEZI JANUARI, 2021.

Hadi kufikia mwezi Januari 31, 2021. Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo imekusanya jumla ya **Tsh. 1,052,454,934.47** kutoka katika vyanzo mbalimbali vya mapato ya ndani sawa na asilimia **70.16** ya **Tsh. 1,500,000,000.00** ya lengo la mwaka. Pia Mapato ya vyanzo lindwa

Halmashauri imekusanya **Tsh. 474,717,390.24** sawa na **39.27%** ya **Tsh.1,208,979,600.00** ya bajeti ya mwaka. Ruzuku ya matumizi ya kawaida (**OC**) hadi mwezi Januari 31,2021 fedha zilizopokelewa ni **Tshs.1,309,873,664.31** sawa na asilimia **41.90** ya lengo la mwaka la **Tsh 3,126,223,360.00**. Fedha za OC zinajumuisha mapokezi ya fedha za Elimu bure kiasi cha **Tshs. 115,374,538.40**, Ruzuku ya Mishahara fedha zilizopokelewa hadi mwezi Januari 31,2021 ni **Tshs.8,595,196,400.00** sawa na asilimia **53.84** ya **Tsh 15,964,966,232.00** ya lengo la mwaka, na Ruzuku ya Miradi ya Maendeleo hadi mwezi Januari 31,2021 imepokelewa kiasi cha **Tsh 1,376,652,523.90** sawa na asilimia **11.14** ya lengo la bajeti kwa mwaka la **Tsh.12,361,811,637.46**

MAKUSANYO YA MAPATO YA NDANI KWA MWEZI JANUARI, 2020.

Kwa mwezi Januari 31,2021 Halmashauri imekusanya kiasi cha **Tshs. 210,620,752.00** kutoka katika vyanzo vya ndani sawa na asilimia **168.50** ya lengo la mwezi la **Tsh. 125,000,000.00**. Halmashauri imekusanya mapato ya vyanzo lindwa kiasi cha **Tshs.107,508,029.19** ya lengo la mwezi la **Tshs.100,748,300.00** sawa na **106.61%**

C. TAARIFA YA MATUMIZI MWEZI JANUARI, 2021.

Katika kipindi cha Mwezi **Julai** hadi **Januari 2021**, Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo katika utekelezaji wa majukumu yake imetumia kiasi cha **Tshs 12,859,955,451.85** sawa na asilimia **36.41** ya **Tshs 35,320,785,583.46** jumla ya makisio ya Mwaka pamoja na salio anzia la Mwaka. Kwa Mwezi Januari 2021 Halmashauri imetumia kiasi cha **TSh 1,684,904,681.54** Kati ya fedha hizo, kiasi cha **Tshs. 99,983,522.00** ni matumizi ya fedha za makusanyo ya ndani, **Tshs.1,210,183,000.00** ni matumizi ya fedha Mshahara kwa mwezi Januari 2021, Kiasi cha **Tshs.19,378,700.00** ni matumizi ya fedha za OC na Kiasi cha **Tshs 193,655,725.00** ni Fedha za Miradi ya Maendeleo.

Nawasilisha.

CPA(T) Edwin J. Magere

Kny: Mkurugenzi Mtendaji

Halmashauri ya Wilaya

KIBONDO